



HALMASHAURI YA WIL KASULU



MWALIKO

ZABUNI KWA AJILI YA KUPANGISHA JENGO KWA AJILI YA HUDUMA YA MGAHAWA (CANTEEN) KATIKA OFISI ZA MAKAO MAKUU YA HALMASHAURI YA WILAYA KASULU

ZABUNI NA. LGA/040/2023/2024/NC/03
06/03/2024

1. Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu inapenda kualika zabuni kutoka kwa watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kutoa huduma ya Mgahawa kutuma maombi yao kwa Zabuni hii.
2. Unalikwa kuwasilisha Zabuni yako kwa ajili ya kupangisha Jengo kwa ajili ya huduma ya Mgahawa kama ilivyoainishwa kwenye Nyaraka za Zabuni. Jengo hili lina viti, meza, TV, Frijii za Vinywaji, Maji, Mfumo wa Maji safi na Maji taka.
3. Waombaji watapewa vitabu vya Zabuni na kupata maelezo ya Zabuni katika Ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi, kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi mpaka saa tisa na nusu (9:30) Alasiri, kwa siku ya Jumatatu mpaka Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko na sikukuu za kitaifa hususani kwa kipindi cha Zabuni hii tu.
4. Zabuni zote katika uhalisia wake (original) pamoja na nakala (copies) mbili (02) zinazofanana zilizojazwa zitawekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa " Namba na Jina la Zabuni." ambazo lazima ziwasilishwe kwa; **Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu**
5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha na kupokea Zabuni ni siku ya **Jumatano ya tarehe 14/03/2024** kabla ya saa nne kamili (4:00) Asubuhi. Hati Zabuni zitafunguliwa hadharani saa nne kamili (4:00) katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu-Nyakitonto ya mbele wawakilishi au Watoa huduma watakoamua kuhudhuria katika ufunguzi wa Zabuni hizo.
6. Kabla ya kujaza na kurudisha Zabuni, mtoa huduma anashauriwa na kusisitizwa kuja kuona jengo linalopangishwa ikiwa na lengo la kumsaidia Muombaji huyu kujaza Zabuni hizi kwa umakini, ukamilifu na usahihi unaokusudiwa.
7. Zabuni zitakazochelewa, zilizowasilishwa sehemu ya Zabuni tu, Zabuni zilizowasilishwa kielektroniki au kwa njia ya posta, Zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa Zabuni, hazitakubaliwa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini kwa hali yoyote ile.


Joseph K. Rwiza,

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
KASULU.**

